



# 53 Samsoni na Wafilisti

## Kwa Biblia

Waamuzi mlango wa 16

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alimpa Samsoni nguvu baada ya kumtii

## Somo

Samsoni alikuwa na nguvu sana. Mungu alikuwa amesema kwamba Samsoni asikunywe divai wala asinyoe nywele. Samsoni alitii Mungu. Hakukunywa divai wala hakunyoa nywele. Mungu alimfanya Samsoni kuwa na nguvu sana. Wafilisti walikuwa adui wa Waisraeli. Samsoni aliongoza Waisraeli. Samsoni alikuwa na nguvu nyingi kushinda Wafilisti. Wafilisti walimchukia na walitaka kumua.

## Samsoni anapenda Delila

Samsoni alipenda mwanamke aitwae Delila. Wafilisti walitaka kujue siri ya nguvu nyingi za Samsoni ili wamue. Kila Mafilisti alikubali kumpa Delila senti kumi na moja za fedha ikiwa atawasaidia kujua siri ya nguvu za Samsoni.

Delila alisisitiza kuuliza Samsoni amwambie mbona alikuwa na nguvu sana. Samsoni hakumwambia. Delila aliendelea kumuuliza. Lakini Samsoni aliendelea kumwambia uongo. Kwanza Samsoni alimwambia kwamba akifungwa kwa nyuzi saba mpya za upinde, ataishiwa na nguvu. Delila alificha Wafilisti ndani ya nyumba yake. Samsoni alipokuwa akilala, Delila alimfunga kwa nyuzi saba mpya za upinde. Alitoa sauti akisema, "Samsoni, Wafilisti wako hapa."

## Maswali

1. Mbona Samsoni alikuwa na nguvu sana?
2. Nani alitaka kuuu Samsoni?
3. Samsoni alimpenda mwanamke gani?
4. Wafilisti walitaka Delila achunguze nini?
5. Samsoni mara ya kwanza aliambia Delila uongo gani?
6. Uongo ingine gani mbili yenye Samsoni aliambia Delila?
7. Nini ilifanyika wakati Samsoni aliambia Delila ukweli?
8. Wafilisti walifanyaje Samsoni?
9. Samsoni alikufa namna gani?
10. Samsoni aliua Wafilisti wangapi alipokufa?

## Majibu


1. Samsoni alikuwa na nguvu kwa sababu alitii Mungu na hakunywa divai wala hakunyoa nywele.
2. Wafilisti walitaka kuuu Samsoni.
3. Samsoni alimpenda Delila.
4. Wafilisti walitaka Delila aulize Samsoni siri ya nguvu yake.
5. Alisema atakuwa dhaifu ikiwa atafungwa kwa nyuzi 7 mpya za upinde.
6. Alisema atakuwa dhaifu ikiwa atafungwa kwa kamba mpya, tena nywele zake zikivumanishwa kwa mtande.
7. Delila alimnyoa nywele, na akapoteza nguvu zake.
8. Wafilisti walimshika, wakamfanya kipofu na kumweka gerezani.
9. Samsoni alikufa alipobomoa guzo za Hekalu.
10. Aliua Wafilisti 3,000.



Lakini Samsoni aliinuka haraka. Alikata zile nyuzi za upinde kwa urahisi sawa na kukata vipande vya pamba na akatoroka.

Delila aliendelea kuuliza Samsoni amwambie siri ya nguvu zake. Samsoni alimwambia kwamba akifungwa na kamba mpya ataishiwa na nguvu. Samsoni alipokuwa akilala, Delila alimfunga kwa kamba mpya. Alitoa sauti na kusema, “Samsoni, wafilisti wako hapa.” Lakini Samsoni alikata kamba na kutoroka.

Delila aliendelea kuuliza Samsoni amwambie siri ya nguvu zake. Samsoni alimwambia akivifumanisha nywele zake katika mtande ataishiwa na nguvu. Samsoni alipokuwa akilala, Delila alifuma nywele zake kwa mtande. Alitoa sauti na kusema, “Samsoni, Wafilisti wako hapa.” Lakini Samsoni aliruka na kutoroka.




Delila alilia na kuendelea kuuliza Samsoni amwambie siri ya nguvu zake. Alisema, “Kama ulinipenda, haungeniambia uongo.”



Mwishowe Samsoni alimwambia ukweli. Mungu alimpa nguvu kwa sababu alitii amri zake. Hajawahi kunyoa nywele zake. Samsoni alipokuwa akilala, Delila alinyoa nywele za Samsoni na kunyoa kichwa chote.

Alipaza sauti na kusema, “Samsoni, Wafilisti wako hapa.” Wakati huu nguvu za Samsoni zilikuwa zimekwisha. Mungu hakukuwa naye. Wafilisti walimshika. Walimfanya kipofu na kumweka gerezani.



### Samsoni anakufa

Nywele za Samsoni ziliendelea kukua alipokuwa gerezani. Siku moja Wafilisti walikuwa na sherehe kubwa kwa Hekalu yao. Walileta Samsoni nje ili wamcheke. Samsoni aliomba Mungu. Aliomba Mungu ampe nguvu ingawaje mara moja tu. Samsoni alishika nguzo mbili za Hekalu. Alivuta hizo nguzo kwa nguvu zake zote. Nguzo zilibomoka na Hekalu ikaanguka chini. Wafilisti elfu tatu waliuwawa. Samsoni naye alikufa. Samsoni aliwa Wafilisti wengi wakati wa kifo chake kuliko wakati mwingine wowote. Kutokea hapo Waisraeli walikuwa na amani kwa muda.

